SWAHILI FORUM 29 (2022): 48-65

UTATA KATIKA UBAINISHAJI WA FASIHI YA WATOTO KWA KUREJELEA KITABU CHA MGOMBA CHANGARAWENI

ALFRED MALUGU

Fasihi ya watoto hujipambanua kwa kupitia sifa mintarafu dhidi ya fasihi ya watu wazima. Miongoni mwa sifa hizi, ni zile zilizobainishwa na wataalamu kama Mulokozi (2017), Schneider (2016), Bakize (2014, 2015), Lynch-Brown na wenzake (2014), Stakic (2014), Matundura na wenzake (2013), na Wamitila (2010); tukiwataja kwa uchache tu. Kwa jumla, wataalamu hawa wanabainisha sifa mahsusi zinazofungamana na kazi za fasihi zinazoingia katika kumbo la fasihi ya Watoto. Kitabu cha *Mgomba Changaraweni* (2005) kilichoandikwa na Ken Walibora kinatambulika kuwa ni miongoni mwa vitabu vya fasihi ya watoto nchini Kenya. Licha ya kitabu hicho kutambuliwa kama fasihi ya watoto, tunaporejelea sifa za fasihi ya watoto kulingana na wataalamu mbalimbali tuliyowataja hapo awali, tunaona kuwa kitabu hiki kina sifa nyingi za fasihi ya watu wazima kuliko fasihi ya watoto. Kwa hivyo basi, tunaonelea kuwa, kitabu hiki kinafaa zaidi kuingia katika kumbo la fasihi ya watu wazima kuliko kuingizwa katika kumbo la fasihi ya watoto. Katika makala haya, tutahakiki kitabu hiki ili kuangalia ni kwa vipi kinaibua utata katika kukubaliana kuwa kinastahili kuwekwa katika kumbo la fasihi ya watoto.

Maneno Muhimu: Fasihi ya watoto, mtoto, saikolojia ya watoto, maadili ya Kiafrika

Utangulizi

Fasihi ya watoto ni uga ambao ulikuwa haujapewa kipaumbele sana katika kushughulikiwa licha ya utanzu huu kuwapo tangu awali. Fasihi ya watoto ilianza kushughulikiwa katika upekee wake huku ikitenganishwa na fasihi ya watu wazima hivi karibuni tu, hususani kuanzia karne ya 18 (Bakize, 2014). Maelezo kama haya tunayapata pia kwa Wamitila (2010), ambaye anadai kuwa, utanzu wa fasihi ya watoto ni utanzu ambao umepuuzwa kwa miaka mingi katika maandishi ya kihakiki. Kazi nyingi za kihakiki hushughulikia fasihi ya watu wazima labda kutokana na imani ya kuwa fasihi ya watoto haistahiki kuchunguzwa kinadharia au inahusu tu ngano za ‘chura na sungura.’ Fasihi ya watoto hurejelea matini au kazi ambazo kimsingi hadhira yake ni watoto. Kutokana na fasihi ya watoto kutokushughulikiwa sana kama ilivyo kwa fasihi ya watu wazima, kumekuwapo jitihada za kuangazia kazi hizi za kifasihi ambazo ni mahsusi kwa watoto. Jitihada hizi zinalenga kuwatazama watoto kama kundi lililokuwa limesahaulika katika kutazamwa kama kundi mahsusi linalohitaji kuwa na fasihi yake mahususi.

Maana ya Fasihi ya Watoto

Ufafanuzi kuhusu fasihi ya watoto unahusishwa na mitazamo mbalimbali. Mitazamo hii, imeweza kutofautiana kutoka mtaalamu mmoja hadi mwingine. Kwa mfano, Ngugi (2012) anafafanua fasihi ya watoto kuwa ni fasihi iliyoandikwa kwa minajili ya kusomwa na watoto.

Kwa upande wake Kahigi (1995), anafafanua kuhusu vitabu vya kundi la watoto ambapo anasema kuwa Mradi wa Vitabu vya Watoto Tanzania unatambua ngazi tatu za vitabu hivyo. Kahigi anaonesha makundi matatu ambapo ngazi ya kwanza ni ile ya awali hadi darasa la pili, ngazi ya pili ni ile ya darasa la tatu hadi la nne na kundi la tatu ni lile la darasa la tano, la sita na saba. Katika ubainishaji huu wa vitabu vya watoto, Kahigi anaonekana kuegemea katika kigezo cha umri hata kama hajasema waziwazi, lakini tunaweza kukadiria umri wa mtoto anayepaswa kuwa katika madarasa tajwa.

Vivyo hivyo, Mulokozi (2017:254) katika kuainisha riwaya, anaainisha kuwa kuna riwaya ya watoto na vijalunga ambapo kwa sheria ya Tanzania, mtoto ni mtu mwenye umri usiozidi miaka 18. Ninaungana na kauli hii ya Mulokozi kuhusiana na mtoto kuchukuliwa kuwa ni mtu mwenye umri usiozidi miaka 18.

Kwa upande wake Wamitila (2010) analifafanua suala la fasihi ya watoto kwa kuliweka katika mitazamo miwili. Mtazamo wa kwanza ni ule wa kuitazama fasihi ya watoto kuwa ni fasihi ambayo hadhira yake ni watoto. Lakini kwa upande mwingine, mtaalamu huyu anadai kuwa fasihi ya watoto ni ile ambayo msingi wa kidhamira na kimaudhui huwarejelea watoto. Kwa upande mwingine, fasihi ya watoto inaweza kufafanuliwa kuwa ni fasihi iliyoandikwa au kusimuliwa na watoto wenyewe[1].

Fasihi ya watoto ni jumla ya vitabu vilivyoandikwa kwa ajili ya watoto, vinasomwa na watoto na/au kuandikwa kuhusu watoto (Schneider, 2016:10). Hata hivyo, mbali na ufafanuzi huu, Schneider (keshatajwa) anaeleza kuwa, yapo mazingira ambayo watoto husoma vitabu vya watu wazima. Anaendelea kwa kutoa maelezo kwamba, kuna wakati kazi za fasihi zinakuwa na ugiligili;

[1] Aidha, tunaonelea kuwa, iwapo fasihi ya watoto ikisimuliwa au kuandikwa kwa mtoto inaweza kukidhi mahitaji ya watoto tofauti na inavyoandikwa na mtu mzima ambaye hujikuta akisahau kuzingatia matakwa ya mtoto kama inavyokusudiwa na kazi za fasihi ya watoto.

kwamba hazioneshi mipaka bayana kwa kuwa kazi husika huweza kujipambanua katika miktadha mbalimbali. Kwa mfano katika *Mgomba Changaraweni*, kazi hii imehusisha sifa za fasihi zote; fasihi ya watu wazima na fasihi ya watoto.

Kulingana na https://www.pearsonhighered.com katika *Introduction to the World of Children's Literature* (n.d.), vitabu vyote vilivyoandikwa kwa ajili ya watoto huwa ni fasihi ya watoto – isipokuwa vitabu kama vya utani, vya katuni, na vitabu ambavyo si vya kibunifu ambavyo havijakusudiwa kusomwa kuanzia mwanzo mpaka mwisho, kama vile kamusi mbalimbali, insaiklopidia, na marejeleo mengine. Baadhi ya watu huichukulia fasihi ya watoto kuwa inahusu watoto walio na umri wa kuanzia kuzaliwa hadi miaka 18. Kwa hivyo, fasihi ya vijana hufafanuliwa kuwa huhusisha umri wa miaka 13 hadi 18 nayo hujulikana kama fasihi ya vijalunga, na fasihi ya vijana kuanzia umri wa kuzaliwa hadi miaka 13 kuwa ni fasihi ya watoto (kur.2-3).

Kwa kuwa fasihi hii imekusudiwa kwa ajili ya watoto, basi hapana shaka kwamba, ni vema hasa ikawahusu watoto wenyewe ikiwa ni pamoja na dhamira zinazozungumziwa zinapaswa ziwalenge watoto. Yafaa zaidi hata yale yanayozungumzwa katika kazi hizo yalenge kuwajenga watoto kuwa na mwelekeo au maadili yanayokubalika katika jamii. Yawezekana hii ndio sababu, ngano nyingi ambazo zipo kwa ajili ya watoto hushindanisha wema na ubaya ambapo daima wema huushinda ubaya.

Kwa jumla, katika kazi hii, tunaichukulia fasihi ya watoto kuwa ni fasihi inayowahusu watu walio na umri wa chini ya miaka 18 lakini wakati huo ikihusisha watoto walio katika umri wa kuwa shuleni, mathalani kuanzia elimu ya msingi. Kwa hivyo, umri unaokadiriwa ni kuanzia miaka 7 hadi 17. Sababu hasa za kuwalenga watoto wa umri huu ni kwa sababu, chini ya umri huu fasihi simulizi ndiyo hasa huwa imepewa kipaumbele. Katika umri huu unaohusishwa na kitabu hiki tunauangazia kwa kuwa ni umri ambao ndio kwanza huwa unaanza kuwekewa msisitizo katika usomaji wa vitabu. Hapa tunamaanisha umri wa kuanzia elimu ya darasa la kwanza na kuendelea. Kwa maana hiyo, ni dhahiri kabisa kwamba, maudhui yanayopatikana katika vitabu lengwa, yanapaswa yachukuane na mahitaji yao lengwa katika jamii, na pia ni sharti yaangazie kusudio la jamii katika kuwafikishia watoto hawa maudhui hayo. Kwa kuzingatia maelezo hayo tuliyoyatoa, basi tunapaswa kukumbuka kwamba, lengo letu katika makala haya, ni kuangazia kundi la watoto

wenye umri wa kuweza kusoma na kuandika na sio la chini ya hapo. Fasihi inayoangaziwa katika kundi hili ni kama vile riwaya, hadithi fupi, tamthiliya au ushairi.

Sifa za Fasihi ya Watoto

Ili kufanikisha malengo ya makala hii, tumerejelea sifa zinazobainishwa na wataalam mbalimbali kuhusiana na kazi za fasihi zinazoweza kutazamwa kama fasihi ya watoto. Wataalam tutakaowarejelea wanapendekeza sifa mintarafu ambazo zinazitofautisha fasihi ya watu wazima dhidi ya fasihi ya watoto. Sifa hizo ndizo hasa zitakazotuongoza katika kukihakiki kitabu cha *Mgomba Changaraweni* na hatimaye kueleza ni kwa nini kitabu hiki kinafaa kutumika kama fasihi ya watu wazima na sio fasihi ya watoto.

Fasihi ya watoto huweza kupambanuliwa kupitia sifa za jumla ambazo zimependekezwa na wataalam mbalimbali. Sifa hizi ndizo hutumiwa kuitofautisha fasihi ya watoto dhidi ya fasihi ya watu wazima. Miongoni mwa wataalam waliobainisha sifa hizi za jumla ni Matundura na Wenzake (2013:30-31), Bakize (2014:6-20), Lyimo (2014:33-43), Lynch-Brown na wenzake (2014:3-4), Stakic (2014:243-251), Schneider (2016:24), Kahigi (1995:21) na pia Mulokozi (2017:254-256). Hawa ni miongoni tu mwa wataalam wachache tuliowarejelea katika kufanikisha ukamilishaji wa makala hii. Watalaam hawa tuliowataja wamefanana katika kutaja sifa hizi tunazoenda kuziorodhesha hapa chini. Sifa hizo ni:

Mosi, hadhira kuu ya kazi ya fasihi ni watoto. Hadhira kuu ya fasihi ya watoto huwalenga watoto wenyewe. Licha ya kwamba vitabu hivi huweza kusomwa hata na watu wazima, lakini watoto ndio huvifurahia zaidi kuliko watu wazima. Mambo yanayowafanya watoto wavifurahie vitabu hivi kuliko watu wazima ni kama vile: picha, lugha rahisi iliyotumika, michezo ya watoto na masuala ya kifantasia. Kazi hizi lazima zizingatie saikolojia ya watoto; yaani mwandishi anapaswa kuandika mada zinazowasisimua watoto, kuwafurahisha, kuepuka kuandika mambo ambayo yatawachukiza watoto au kuwaletea athari hasi na huku zikitumia wahusika bapa. Aidha, hutumia lugha iliyochujwa na kurahisishwa kulingana na ngazi ya wasomaji waliokusudiwa; lugha hiyo huwa na maneno mepesi na yale magumu huelezwa katika sehemu ya mwisho inayojulikana kama

sherehe pamoja na sentensi fupifupi. Katika kazi za fasihi ya watoto, mwandishi anapaswa atumie lugha rahisi itakayowafanya watoto waweze kuelewa maudhui ya kitabu husika.

Pili, watoto ndio nguli na wahusika wakuu (Ngugi, 2012)[2]. Sababu za kutumia watoto ambao ndio nguli na wahusika wakuu inatokana na kuwa, watoto hufurahia sana wanapowaona watoto wenzao wakiwa watendaji kutokana na huvutiwa sana na tabia za wahusika.

Tatu, huwa na visa vichache na ambavyo huwa si changamani, lengo hasa kuwa ni kutomchanganya mtoto na hivyo kushindwa kufuatilia ujumbe uliokusudiwa kutolewa na mwandishi. Hii humrahisishia mtoto kuweza kukifuatilia kisa kimoja kuanzia mwanzo hadi mwisho bila kuingiliwa na kisa kingine.

Nne, hujengwa katika msuko sahili wa matukio. Msuko katika fasihi ya watoto huwa ni sahili. Msuko huu huvifanya visa vitokee kimfuatano na hivyo kumrahisishia mtoto kufuatilia kisa kimoja baada ya kingine. Katika msuko huu, wahusika huwa hawaelezwi kwa kina, wala kwa mapana, na badala yake, vitendo halisi vya wahusika, yakiwepo maneno wanayoyasema wao ndio yanayojenga kisa chenyewe.

Tano, hutumia sana fantasia. Bakize (2014) anafafanua fantasia kuwa ni mbinu ya kuchangamanisha matukio halisi na yale yasiyokuwa halisi katika kazi ya fasihi. Mbinu hii Senkoro (2006) ameiita uhalisiamazingaombwe. Ni mbinu inayoelezea mambo yaliyo nje ya uhalisi. Watoto huvutiwa sana na mambo ya ajabuajabu ambayo hayawezekani kutokea katika ulimwengu halisi. Kutokana na matumizi ya mbinu hii, watoto hawaishii kufurahia tu hadithi bali hujifunza mambo mbalimbali kama vile ya kujiamini, ushujaa, upelelezi na udadisi (Bakize, 2014:16).

Sita, mambo mema ndiyo yatarajiwayo. Katika kazi za fasihi ya watoto, wema na ubaya hupambanishwa ambapo daima wema hushinda.

Saba, hukusudiwa kutoa mafundisho au maadili kwa kutoa mifano. Sehemu kubwa ya fasihi ya watoto hukusudiwa kuwapa maadili watoto, yaani kipi wafuate na kipi wakiepuke. Miongoni mwa

[2] Ngugi (2012:22) akimnukuu Huck (1979), anasema kuwa, sifa moja kuu ya fasihi ya watoto ni kule kutumia wahusika ambao ni watoto, huku mhusika mkuu akiwa ni mtoto. Watoto hufurahia wahusika ambao wanaweza kuwaamini, kujitambulisha na kujinasibisha nao na hata kuwaelewa.

mambo ambayo wanaadilishwa kuyaepuka ni kama vile uchoyo, ulafi, ukaidi, uvivu, wivu, wizi na kadhalika. Kwa jumla, huepuka kusawiri matukio hasi kama ya mauaji yaliyokithiri, uhalifu mkubwa, uzinzi na uasherati, ngono za waziwazi, n.k. Matukio haya huepukwa na waandishi kwa sababu mambo haya yanaonekana hayana mchango mkubwa sana kwa watoto kwani kazi hizi hukusudiwa zaidi kujenga maadili mema kwa watoto. Kwa hivyo, matukio kama haya yanaweza kuwaogofya ama kutowajenga kimaadili.

Nane, mwega wa kidhamira huwa ni watoto wenyewe. Dhamira katika kazi za fasihi ya watoto huelekezwa katika kuwanufaisha ama kuwajenga watoto kulingana na malengo ama maadili ya jamii zao. Kwa hivyo, dhamira zinazochukuana na mahitaji ya watoto katika jamii ndizo hupendekezwa kuangaziwa katika vitabu hivyo.

Tisa, huelemea kwenye ramsa (mwisho mwema) kuliko tanzia. Fasihi ya watoto hujiepusha na hitimisho lenye kuhuzunisha na badala yake hujikita katika kuwapa ushindi wahusika wakuu ambao mara nyingi hukusudiwa kuwa ni watoto.

Kumi, kazi nyingi zimejengwa kwa motifu ya safari na msako. Motifu ya safari na msako hujengwa katika mazingira ambayo toka mwanzo mhusika anasafiri kwa lengo la kusaka/kutafuta kitu fulani. Ni kutokana na motifu hii ya safari na msako ambavyo kwa pamoja humjengea hamu msomaji kutaka kufahamu hatima ya kile kinachosakwa.

Kwa jumla, wataalam tuliowataja wanakubaliana na sifa hizo. Licha ya kuwa sio lazima sifa zote hizo ziwepo katika kazi ya fasihi ya watoto, lakini ni muhimu nyingi ya sifa zinapaswa kujitokeza katika kazi husika. Kutofautiana kwa umri wa watoto kunaweza kutofautisha ulazima wa sifa fulani hitajika kutoka kundi moja hadi jingine. Kwa mfano, sifa za ulazima wa kuwapo michoro, motifu ya safari na msako na matumizi ya fantasia/uhalisiajabu, huweza kuwafaa zaidi watoto wenye umri wa kati ya miaka 5 hadi miaka 12. Sifa hizo nyingine zilizobaki zinaweza kuzingatiwa kwa ujumla wake pasipo kutenga kundi mahsusi kwani ni muhimu kuzingatiwa kwa makundi hayo yote. Vilevile, licha ya kuwa sio lazima sifa zote zijitokeze katika kazi ya watoto ndipo ichukuliwe kuwa fasihi ya watoto, ni muhimu walau kuwe na sifa hata nusu ya hizo zilizotajwa. Kwa mfano ni muhimu dhamira ziwe za kuigwa na watoto. Visa visiwe vingi sana,

kusiwe na matukio ya kutisha ama kukatisha tamaa kama vile kujiua/mauaji ya kutisha, vitendo vya kushiriki mapenzi katika umri mdogo, lugha rahisi itumike na pia mhusika mkuu ambaye atakuwa ni sawa na kundi lengwa la fasihi hii na pia aonyeshe mfano wa kuigwa kwa wasomaji wa kazi husika.

Muhtasari wa Kitabu cha Mgomba Changaraweni

Mgomba Changaraweni ni kitabu kilichoandikwa na Ken Walibora na kuchapishwa kwa mara ya kwanza (2004) kabla ya kuchapishwa tena (2005), (2006) na (2007). Kitabu hiki kinawazungumzia hasa wahusika wawili ambao ni Chongameno na Alice Kesho. Chongameno ni kijana mwenye umri wa yapata miaka 23. Kwa upande wake Alice Kesho, Alice alikuwa ni msichana mwenye umri wa miaka 16 wakati ambapo alipomwandikia barua Chongameno. Katika hali ya suitafahamu, Alice Kesho anampenda Chongameno na hivyo kutamani Chongameno awe mtu atakayeishi naye katika maisha yake kama mume wake. Alice Kesho anajaribu kutumia kila njia ili aweze kumpata Chongameno lakini Chongameno anaonekana hayupo tayari kuoana na Alice Kesho. Binti huyu ni wa familia ya kitajiri ilhali Chongameno akiwa anaishi maisha ya ufukara wakati huo akiwa ameajiriwa kuchunga mifugo kwa ujira wa kijungu jiko tu. Huenda hali hii ya kuwa fukara ilimfanya Chongameno aone kama hastahili kuoana na Alice Kesho. Miaka sita baadaye, baada ya Alice kutumia mbinu zote ili kumpata Chongameno kushindikana ndipo kwa hasira anaamua kuchoma moto msitu wa Suwerwa, msitu ambao Chongameno alikuwa akichungia mifugo humo. Hali ya moto kuteketeza msitu wa Suwerwa ulizua taharuki kwa wakazi wa kijiji cha Sangura na vijiji vya jirani. Chongameno alijaribu kuuzima moto uliokuwa unawaka bila mafanikio. Wanakijiji walijitahidi kwa kila namna kuuzima moto huo bila mafanikio. Waliamini kuwa, kwa kuwa moto umewashinda kuuzima, basi walau aliyeuwasha asingeliweza kuwashinda.

Nguvu kubwa alizozitumia Chongameno kuuzima moto bila mafaniko zilimfanya aishiwe nguvu na hatimaye kuzirai. Watalii walimuokota na kumpeleka hospitali ya Kapsara akiwa hajijui wala hajitambui. Chongameno alipelekwa hospitalini na askari waliokuwa wanamtafuta na hivyo kuwekwa chini ya ulinzi wa askari wakati akiendelea kupata matibabu. Baada ya kupona, Chongameno alifikishwa mahakamani na kuhukumiwa kifungo cha miaka mitano na viboko viwili. Baada ya kutumikia kifungo kwa siku kadhaa, aliachiliwa huru, na hii ni baada ya uchunguzi

uliofanywa na polisi na kubaini kuwa Chongameno siye aliyechoma msitu huo. Alipotoka jela, alipokelewa na umati wa watu wa kijiji cha Sangura akiwemo mzee Juma Kesho ambaye ni baba wa Alice Kesho. Mzee huyu alimuomba radhi Chongameno kwa adhabu aliyoadhibiwa kwa kosa lililofanywa na Alice. Baada ya kuomba radhi, mzee huyo alitoa karatasi ndogo na kumpatia Chongameno karatasi iliyoonesha kabisa kuwa Alice alikuwa ameamua kujiua baada ya kuona kwamba ndoto yake ya kuolewa na Chongameno ni kama imefifia. Pia aliamua kujiua baada ya nafsi kumsuta kwa kumsababishia Chongameno kufungwa kwa kosa ambalo hakulitenda.

Utata Unaojitokeza katika Kubainisha Kitabu cha *Mgomba Changaraweni* kama Mojawapo ya Kazi za Fasihi ya Watoto

Katika kuelezea utata unaojitokeza katika ubainishaji wa kitabu cha *Mgomba Changaraweni* kama mojawapo ya kazi za fasihi ya watoto, tutashughulikia kipengele hiki kwa kutanguliza sifa fulani ya fasihi ya watoto na kisha ndipo malezo yanayohusiana na uchambuzi wa kazi husika yatakapofuata. Aidha, tunapaswa kufahamu kuwa, kitabu hiki cha *Mgomba Changaraweni* kimewekwa katika orodha ya vitabu vinavyopaswa kusomwa na wanafunzi wa darasa la 7 na 8. Wanafunzi wa madarasa haya nchini Kenya hukadiriwa kuwa na umri wa kati ya miaka 12 hadi 13.

Kwanza, utata unaanzia katika mambo yanayowafanya watoto wavifurahie vitabu hivi kuliko watu wazima ambayo ni kama vile: picha, lugha rahisi iliyotumika, michezo ya watoto na masuala ya kifantasia. Stakic (2014) anaeleza kuwa, lugha inayotumiwa katika uandishi wa fasihi ya watoto inapaswa iwe ya kuvutia ili kuwafanya watoto watamani kuendelea kusoma kazi husika. Matumizi ya maneno magumu ama misamiati huweza kutomshawishi mtoto kuendelea kutamani kuisoma kazi husika. Kama nukuu inavyoonesha hapo chini, kuna sehemu mwandishi ametumia misamiati na misemo migumu tena pasipo kuitolea maelezo katika sehemu ya sherehe. Hali hii inaweza kumtatiza msomaji katika kuelewa hicho kinachozungmziwa na ndipo hasa, Mulokozi (2017) alisisitiza pawepo na ukurasa wa sherehe mwisho kwa ajili ya kutolea ufafanuzi maneno, misamiati au misemo ambayo inaweza kuwa migumu kueleweka kwa watoto. Misamiati na misemo iliyoandikwa katika hati mlazo ni mifano ya lugha inayodhihirisha ugumu kueleweka kwa mtoto pindi anaposoma kitabu hiki. Kwa mfano:

> … Mathalan kuna wasemao alizaliwa Morogoro katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mama aliyekuwa na *midomo mitatu na titi moja* (uk. 8) (Msisitizo ni wa mwandishi wa makala).
>
> Alice alikataa *abadan katan* na kushinda akilia mchana kutwa na kukesha vivyo hivyo usiku kucha (kur. 19-20) (Msisitizo ni wa mwandishi wa makala)
>
> Kama kawaida wazee wake hawakumzuilia haja. *Hawakuwa majoka ya mdimu yanayochunga watundao* (uk. 21) (Msisitizo ni wa mwandishi wa makala).
>
> Watu wote wa Sangura *waliapa ima fa ima*, wangemsaka aliyewasha moto huo ili *apate cha mtema kuni*… Watu wa Sangura walikuwa na *ghera na ghamiza* si haba. (uk. 33) (Msisitizo ni wa mwandishi wa makala).

Hata hivyo, mwandishi amezingatia suala la matumizi ya picha ambapo katika kitabu hiki kuna picha mbalimbali zinazoshadidia baadhi ya maelezo yaliyotolewa. Kutokana na matumizi ya picha alizozitumia mwandishi katika kitabu hiki, mwandishi amesawiri vema sifa inayosisitiza kitabu cha fasihi ya watoto kuhitajika kuwa na picha. Kama tulivyosema hapo awali, watoto huvutiwa sana na michoro ama picha. Michoro na picha hizi humvutia na kumshawishi mtoto ili ashawishike kusoma kitabu. Picha hizi zinapatikana kuanzia kwenye jalada la kitabu, uk.12, 17, 22, 27, 30, 36, 42, 46, 49, 52, 60 na 71.

Pia kazi hizi lazima zizingatie saikolojia ya watoto. Kazi zisizozingatia saikolojia au mahitaji ya watoto zinaweza zisiwahamasishe watoto kupenda kusoma vitabu hivi. Mojawapo ya mada zinazozungumziwa humu ni mada ya mapenzi. Mapenzi haya yanahusisha mahusiano baina ya mwanamke dhidi ya mwanaume. Ujumbe wa Alice kwenda kwa Chongameno unatudhihirishia maelezo tuliyoyatoa. Mwandishi anasema:

> Sahibu Chongameno,
>
> Mbona unajirahisi hivyo? Utasema wewe ni maskini. Hilo mimi silikani asilani. Lakini niambie: ni mali gani iliyo na thamani bora zaidi ya adabu njema? Ni mali gani inayozidi utamu wa mapenzi bora? ... (uk. 11).

Kwa maoni yetu, katika kitabu hiki, mwandishi ametumia mada ambayo pengine inaweza isiwafurahishe sana watoto; mada ya mapenzi. Mada za namna hii katika fasihi pendwa huzichukulia kama huwa zipo kwa ajili ya kuburudisha tu huku zikiwa na nafasi ndogo ya kuelimisha. Kwa jumla, mada za namna hii huwa sio kipaumbele cha watoto.

Pili, watoto kama nguli (wahusika wakuu ambao katika kazi ya fasihi humalizika huku wao ndio wakiwa washindi). Katika kazi ya fasihi ya watoto, licha ya wahusika wakuu kutarajiwa kuwa ni

watoto, inatarajiwa kwamba kazi husika inapaswa imaliike kwa kuonesha ushindi kwa mhusika mkuu ambaye ni mtoto na siyo kinyume chake. Utata mwingine unajitokeza hapa ambapo watoto ndio wanapaswa kusawiriwa kuwa wahusika wakuu katika fasihi ya watoto. Katika kitabu hiki, wahusika wakuu wanaosawiriwa sio watoto, kwani wana umri wa zaidi ya miaka 18. Kuthibitisha hili, mwandishi anasema:

> Alice amesoma mpaka kidato cha nne, katika mojawapo ya shule za kitaifa nchini. Yuangoja kwenda katika Chuo cha Waalimu cha Kaimosi (uk. 14).
>
> Kwa hakika sura yake ilikuwa ya kutamanisha na kuvutia. Wengi waliania uchumba naye kutokana na hilo, lakini aliwakatalia mbali. Siku moja mathalan alikuja mwanasheria mmoja kutoka Nairobi, kuleta posa kwa wazee wake Alice. Alikuja na Benz moja lenye fahari na kupokelewa kwa vifijo na nderemo. Lakini Alice alikataa abadan katan na kushinda akilia mchana kutwa na kukesha vivyo hivyo usiku kucha (kur. 19-20).
>
> Chongameno ni kijana mwanaume mwenye umri wa yapata miaka ishirini na mitatu. Ana ngozi nyeusi kama kizimwili na ndani ya kifua chake kipana mna moyo mweupe pe. Shungi la nywele zake za kipilipili lachukuana vizuri na ngozi yake nyeusi. Chongameno ni kijana mwenye nguvu nyingi na kidari chake kimetutumka. Lakini pengine linalotamanisha zaidi ni mtazamo wake na tabasamu lake. Mtazamo huo na tabasamu hilo ni kama sumaku inayompa mvuto mbele ya wasichana wengi wasiweze kujizuia kumtamani (uk. 9).
>
> Mtu mmoja aliyewasha moto ulioteketeza msitu, nyumba tano na mamia ya mifugo katika kijiji cha Sangura, amepatikana amelazwa katika hospitali ya wilaya ya mjini Kapsara. Mtu huyu mwenye umri zaidi ya miaka 20 yasemekana yuko katika hali mahututi (uk. 43).

Kutokana na nukuu hizo hapo juu, ni dhahiri kabisa wahusika waliotumika hawakuwa watoto (hawakuwa na miaka chini ya kumi na nane) bali walikuwa ni watu wazima. Alice kwa mfano, tunaambiwa alikuwa amemaliza kidato cha nne na anajiandaa kujiunga na chuo cha walimu cha Kaimosi. Wakati huohuo tunaonyeshwa kuwa Alice alikuwa ameishaanza kuchumbiwa. Ni dhahiri kabisa msichana aliyemaliza kidato cha nne na wakati huo akiwa tayari kuchumbiwa, basi hapana shaka kabisa atakuwa ni mtu ambaye ana miaka siyo chini ya 18. Vivyo hivyo umri wa Chongameno unatajwa kabisa kuwa ana umri wa miaka zaidi ya 23. Kama tulivyoona katika maelezo ya sifa za fasihi ya watoto, matumizi haya ya wahusika ambao tayari ni watu wazima hayawezi kuwavutia zaidi watoto kama ambavyo wangetumika watoto.

Tatu, huwa na visa vichache na ambavyo huwa si changamani, lengo hasa huwa ni kutomchanganya mtoto na hivyo kushindwa kufuatilia ujumbe uliokusudiwa kutolewa na

mwandishi. Hii humrahisishia mtoto kuweza kukifuatilia kisa kimoja kuanzia mwanzo hadi mwisho bila kuingiliwa na kisa kingine. Sifa hii pia haijajitokeza katika kitabu hiki cha *Mgomba Changaraweni* kwani dhamira zake zimechanganywa sana; hazijazingatia mtiririko wa kuanza na kisa kimoja kikaelezewa hadi mwishoni ndipo kikaingizwa kisa kingine, bali chenyewe kimeenda kinachanganya visa. Kwa mfano, maelezo yanayoelezwa kuhusu barua aliyoipokea Chongameno kutoka kwa Alice uk. 9 yanakatishwa kwa kuingiliwa na maelezo kuhusu hali ya hewa ilivyokuwa katika eneo la Sangura. Maelezo kuhusu barua hiyo tunayakuta tena yameendelezwa kur. 11-14. Maelezo kuhusiana na barua aliyoipokea Chongameno yalipaswa yaunganishwe bila kukatishwa. Ili kuweka mwendelezo wa kisa, ilipaswa maelezo kuhusu barua aliyoipokea Chongameno uk. 9 yangeunganishwa na maelezo yanayohusu barua inahusu nini kur. 11- 14 kisha maelezo yaliyopo uk. 9 aya ya mwisho na mwendelezo wake kur. 10 – 11 kabla ya kufika aya ya mwisho ndipo yafuate. Hebu tuone mfano wa mpangilio huo:

> Barua aliyoipokea ilimfikirisha sana Chongameno. Moyo wake ulituta kwa wasiwasi na kiwewe. Alighumiwa asijue la kufanya (uk. 9)
>
> Ilikuwa alasiri; jua la kiangazi lilikuwa haliangazi bali launguza. Joto lilikuwa linahanikiza kila pembe… Chongameno alikuwa machungani. Ng'ombe wa Mzee Masaba aliowachunga walikuwa wamekonda vibaya… na tajiri Masaba akijua Chongameno kamwachia ndama kunyonya na kumkosesha maziwa atamwadhibu kwa kumkata mshahara (kur. 9-11)
>
> Kisha aliitoa mfukoni tena ile barua iliyomfadhaisha mno. Akaikunjua na kuanza kuisoma tena. Alipenga kamasi kwa mkono mmoja na chozi likamtoka. "Sahibu Chongameno, mbona unajirahisi hivyo? Unasema wewe ni maskini. Hilo mimi silikani asilani. Lakini niambie: ni mali gani iliyo na thamani bora zaidi ya adabu njema?... (kur. 11-14).

Hali hii ya kuchanganya visa pia tunaiona (kur. 15-21) na pia hata unapoanzia (uk. 21) napo kuna mchanganyo huu wa visa unaoweza kumchanganya mtoto.

Nne, hujengwa katika visa sahili. Kitabu hiki hakijazingatia sifa hiyo na kwa hivyo kinaweza kumchanganya msomaji. Mpangilio wa visa katika kitabu hiki ni wa kiuchangamano au rejea/rukia. Hapa tunaona visa vimechanganywa sana hali inayoweza kumpotosha au kumkatisha tamaa mtoto anayesoma kitabu hiki. Tukiangalia maelezo kuhusu wasifu wa Chongameno yanayopatikana uk. 9 yalipaswa yayatanguliye maelezo kuhusu asili ya jina "Chongameno" katika kur. 7-8 kwani ilipaswa tuelezwe kwanza Chongameno alikuwa ni mtu wa aina gani (wasifu wake) na kisha ndipo

tuelezwe jina hilo la Chongameno lilitoka wapi kinyume na ilivyopangiliwa katika kitabu hiki. Hebu tuangalie muundo uliotumika jinsi unavyosawiri kutokuwapo kwa usahili:

> Chongameno. Hivyo ndivyo anavyojulikana na watu wote wamjuao. Na wamjuao sio wachache. Jina lake hili la msimbo, Chongameno limesambaa ndani na nje ya kijiji cha Sangura kama vile moto katika kichaka kikavu. Hata hivyo, haijulikani bayana kama jina hili la mzaha, Chongameno, alipewa na watu au kajipa mwenyewe… Ni vigumu kujua kama jina lake halisi ni Kamau, Wanjala au Otieno. … Si ajabu basi kwa kuficha siri ya asili yake kumewapa wazushi nafasi ya kuzua hadithi mbalimbali kuihusu asili yake hiyo (kur. 7-8).
>
> Chongameno ni kijana mwanaume mwenye umri wa yapata miaka ishirini na mitatu. Ana ngozi nyeusi kama kizimwili na ndani ya kifua chake kipana mna moyo mweupe pe. Shungi la nywele zake za kipilipili lachukuana vizuri na ngozi yake nyeusi. Chongameno ni kijana mwenye nguvu nyingi na kidari chake kimetutumka. Lakini pengine linalotamanisha zaidi ni mtazamo wake na tabasamu lake. Mtazamo huo na tabasamu hilo ni kama sumaku inayompa mvuto mbele ya wasichana wengi wasiweze kujizuia kumtamani (uk. 9).

Vilevile, kuna ukatishwaji wa kile kilichokuwa kinaelezwa hapo awali na ikaingizwa simulizi nyingine. Hali hii inaweza kumchanganya mtoto na hata kumfanya asishawishike kuendelea kusoma kitabu. Katika uk.9 kuna maelezo kuhusu Chongameno kupokea barua lakini kabla ya kuelezwa barua hiyo ilikuwa imetoka kwa nani na ilihusu nini, simulizi hiyo inakatishwa na aya inayofuata tu inaanza kwa kuelezea kuhusu mambo mengine kabisa. Maelezo kuhusu barua aliyoipokea Chongameno yanakuja kuendelea tena katika kur. 11-13. Hebu tuone jinsi mchangamano huu unavyojitokeza:

> Barua aliyoipokea ilimfikirisha sana Chongameno. Moyo wake ulituta kwa wasiwasi na kiwewe. Alighumiwa asijue la kufanya.
>
> Ilikuwa alasiri; jua la kiangazi lilikuwa haliangazi bali launguza. Joto lilikuwa lihanikiza kila pembe. Lau kama ungaliona jinsi ukame ulivyofuma eneo lote la Sangura, ingalikuwa vigumu kwako kusadiki kwamba kumewahi kunyesha walau tone moja la mvua tangu gharika ya Nuhu. … (kur. 9-10)
>
> … Kisha aliitoa mfukoni tena ile barua iliyomfadhaisha mno. Akaikunjua na kuanza kuisoma tena. Alipenga kamasi kwa mkono mmoja na chozi likamtoka (uk.11).
>
> Baada ya kumaliza kuidurusu hiyo barua Chongameno aliikunja tena na kuirudisha mfukoni. Huyu mwanamke anitakiani? Alijiuliza (uk.13).

Tano, mambo mema ndiyo yatarajiwayo. Katika kazi za fasihi ya watoto, wema na ubaya hupambanishwa ambapo daima wema hushinda. Fasihi ya watoto hutarajia kuwaelekeza watoto mambo mema. Huonyesha pia kuwa, pindi wema na uovu unapopambanishwa, basi wema

hushinda. Sifa hii walau imejitokeza katika kitabu hiki cha *Mgomba Changaraweni*. Katika kitabu hiki tunaona kuwa, Chongameno anafungwa kwa kudhaniwa kuwa ndiye aliyechoma msitu. Anahukumiwa kifungo cha miaka mitano na viboko viwili. Lakini baada tu ya muda mfupi tangu ahukumiwe inakuja kubainika kuwa kumbe sio yeye aliyechoma msitu wa Suwerwa na hivyo kuachiwa huru. Mwandishi anatwambia:

> Hamaki zilimpanda hakimu. Alimtazama Chongameno kwa macho makali kama ya simba. Kisha akaendelea kutoa hukumu yake. Chongameno angefungwa miaka mitano jela na kucharazwa viboko viwili kwa kusababisha moto ulioteketeza mali ya serikali na wakaaji wa Sangura (uk. 64).
>
> Chongameno alikuwa amemaliza wiki mbili katika gereza. Jela kuna hali ngumu, lakini haikuwa peke yake. … alikuwa kazoea sulubu. Alikuwa anaomba dua aimalize miaka yake mitano salama salamini. Ndipo siku moja akaupata mshangao ambao hatausahau maishani mwake. Aliitwa na askari jela mara baada ya kiamshakinywa. Alisindikizwa moja kwa moja hadi katika ofisi ya mkuu wa jela Bwana Mabonga. Kisha aliambiwa kuwa uchunguzi uliofanywa ulikuwa umethibitisha kuwa yeye hakuwa na hatia na kwa hivyo angeachiliwa huru (kur. 68-69).

Saba, hukusudiwa kutoa mafundisho au maadili kwa mifano. Sehemu kubwa ya fasihi ya watoto hukusudiwa kuwapa maadili watoto, yaani kipi wafuate na kipi wakiepuke. Miongoni mwa mambo ambayo wanaadilishwa kuyaepuka ni kama vile uchoyo, ulafi, ukaidi, uvivu, wivu, wizi na kadhalika. Katika kitabu hiki cha *Mgomba Changaraweni*, tunaona pia sifa hii inakosekana. Kitendo cha Alice Kesho kuchoma moto msitu na kusababisha hasara kubwa kwa wakazi wa kijiji cha Sangura ni kinyume na maadili ya jamii. Ni kitendo ambacho hakipaswi kuigwa. Kadhalika, kitendo cha Alice kujiua nacho ni kinyume na maadili. Mwandishi anatuthibitishia matukio haya kama ifuatavyo:

> Bafuni alikuwa ametumia takribani masaa matatu. Sabuni aliyoitumia ilibaki bapa ndogo na nyembamba kama kijikaratasi. Na hilo lisionekane ni ajabu, maana hiyo ni desturi yake (uk. 18).
>
> "Wajua Chongameno, nalia kwa sababu wewe unaumia bure bilashi. Wewe hukuwasha ule moto. Wallahi wewe unaumia bure. … mimi ndiye niliyeee…uwasha moooto u-ule. Sijamwambia mtu mwingine." (uk. 61).
>
> Alice alikuwa kanywa sumu. Alipatikana chumbani mwake akiwa mahututi. Wazazi walimkimbiza hospitalini lakini sumu ikamzidi. …Chongameno alipofika Sangura aliweka shada la maua kwenye kaburi la marehemu Alice. Machozi yalimtoka njia nne akalia kama mtoto mdogo (uk. 72).

Kimsingi, kulingana na maadili ya Kiafrika sio sahihi sana kutumia muda mwingi kuoga (saa tatu kwa kuoga tu!). Aidha, tukio la kuchoma moto msitu uliyosababisha adha na uharibifu mkubwa wa mali za watu ni kinyume cha maadili anayopaswa kuwa nayo mtu. Sanjari ya maelezo hayo, kitendo cha kuamua kujiua nacho hakikubaliki kabisa katika utamaduni wetu. Tulitarajia katika sehemu hii mwandishi aoneshe hali ya kukemea vitendo hivi ili vionekane havikubaliki katika jamii. Kwa kutokukemea vitendo hivi, watoto wanaweza kudhani kwamba suluhu ya kukataliwa ni kujiua ama kuharibu mali ya umma kwa sababu tu ya matamanio yao ambayo hayakufanikiwa kutokana na mtu fulani. Tunatarajia kazi ya fasihi ya watoto iwape watoto tumaini jipya hata pale wanapokumbana na mambo magumu na sio kukata tamaa na kujiua. Kwa mfano, je, watoto wajifunze kwamba suluhu ya kutofikiwa kwa matarajio yao ni kujiua ama kuharibu mali ya umma?

Nane, Huepuka kusawiri matukio hasi kama ya mauaji yaliyokithiri, uhalifu mkubwa, uzinzi na uasherati, ngono za waziwazi, n.k. Sifa hii inakosekana katika kitabu hiki kwani mwandishi amesawiri matukio hasi. Watoto huwafurahia wahusika wanaoonyesha mifano ya kipekee kama vile kuwa thabiti, ujasiri, kutenda haki, kuwa na maadili, na pia kuwa na busara (Stakic, 2014:247). Katika kitabu hiki, Alice hatuonyeshi mfano bora unaopaswa kuigwa na watoto. Hii ina maana kwamba, je, watoto wanapokumbana na masahibu mazito suluhu yake iwe ni kujiua? Au kuharibu mali ya umma? Yapo matukio kadhaa yanayowasibu wanafunzi yanayosababisha watoto kuchukua maamuzi ya kujiua. Matukio kama vile kupata mimba au kushindwa mtihani huweza kusababisha baadhi ya watoto kuchukua maamuzi ya kujiua. Kazi ya fasihi ya watoto inapaswa ionyeshe kukemea matukio ya kujiua ama kukata tamaa. Hata pindi inapotokea mtoto ameanguka kwa kuchukua maamuzi yasiyofaa, basi awepo mwingine ambaye ataonyesha mfano wa kuigwa ili kuwapa moyo wasomaji. Hali hii ni tofauti na tunavyosawiriwa katika kitabu cha *Mgomba Changaraweni*. Tukio hasi mojawapo linalosawiriwa na kitabu hiki ni hilo la Alice kujiua. Vilevile, tukio hasi jingine linalosawiriwa katika kitabu hiki ni lile la Alice Kesho kuamua kuuteketeza kwa moto msitu wa Suwerwa. Kitendo cha kuuchoma moto msitu huu ni dhamira hasi ambayo haipaswi kuigwa na watoto. Mwandishi anatwambia:

"Wajua Chongameno, nalia kwa sababu wewe unaumia bure bilashi. Wewe hukuwasha

> ule moto. Wallahi wewe unaumia bure. … mimi ndiye niliyeee…uwasha moooto u-ule. Sijamwambia mtu mwingine." (uk. 61).
>
> Alice alikuwa kanywa sumu. Alipatikana chumbani mwake akiwa mahututi. Wazazi walimkimbiza hospitalini lakini sumu ikamzidi. …Chongameno alipofika Sangura aliweka shada la maua kwenye kaburi la marehemu Alice. Machozi yalimtoka njia nne akalia kama mtoto mdogo (uk. 72).

Tisa, mwega wa kidhamira huwa ni watoto wenyewe. Fasihi ya watoto inakusudiwa dhamira zake ziwalenge watoto wenyewe. Sifa hii pia inakosekana katika kitabu hiki kwani dhamira zinazozungumziwa katika kitabu hiki haziwalengi watoto bali watu wazima. Kwa mfano, je, watoto wanajifunza nini kwa kitendo cha Alice Kesho kulazimisha kumpenda Chongameno ilhali Chongameno mwenyewe alikuwa ameishaonyesha kutomtaka Alice (kur. 24-26)? Au watoto wanajifunza nini kwa kitendo cha Alice kumkuta Chongameno akiwa anaoga ghafla naye akavua nguo na kujitosa kwenye maji (uk. 24)? Zaidi ya haya, tunaambiwa Alice alikuwa akiingia bafuni anatumia takribani saa tatu kwa kuoga tu. Je, watoto wanajifunza nini hapa? Je, nao wanapaswa wawe wanatumia takribani saa tatu kwa kuoga tu?

Kumi, huelemea kwenye ramsa (mwisho mwema) kuliko tanzia. Inakusudiwa kuwa, kazi yoyote ya fasihi ya watoto kujiepusha na mwisho wa kuhuzunisha (tanzia) bali mwisho mwema, mwisho wenye matumaini au mafanikio (ramsa). Tofauti na sifa hii, kitabu hiki cha *Mgomba Changaraweni* hakichukuani na sifa hii kwani kimeishia kwa tanzia badala ya ramsa. Wahusika wote wawili wanaishia kwenye majonzi kwani Alice anaamua kujiua lakini Chongameno naye anaishia kulia kama mtoto mdogo kutokana na kifo cha Alice. Haya tunaweza kuyathibitisha kama ifuatavyo:

> Alice alikuwa kanywa sumu. Alipatikana chumbani mwake akiwa mahututi. Wazazi walimkimbiza hospitalini lakini sumu ikamzidi. …Chongameno alipofika Sangura aliweka shada la maua kwenye kaburi la marehemu Alice. Machozi yalimtoka njia nne akalia kama mtoto mdogo (uk. 72).

Kumi na moja, kazi nyingi zimejengwa kwa motifu ya safari na msako. Sifa hii imejitokeza kupitia msako katika kazi hii ya *Mgomba Changaraweni* ijapokuwa msako huo unaofanyika haukuwa na mafaniko. Katika kitabu hiki, hakuna motifu ya safari bali kuna msako tu. Hakuna mhusika anayesafiri kwa lengo au malengo fulani. Kwa upande mwingine, msako usio na mafanikio wenyewe unaonyeshwa na mhusika Alice ambaye yeye alilisaka penzi la Chongameno

kwa muda mrefu bila mafanikio. Msako huu unaishia kwa mhusika kukata tamaa ambapo hatimaye anaamua kujiua. Msako huu tunaonyeshwa ulianzia pale Alice alipomkuta Chongameno akiwa anaoga naye akajitosa majini kumfuata Chongameno (uk. 24). Haikuishia hapo, Alice anamwandikia barua Chongameno akimtaka wawe na mahusiano. Zaidi ya hayo, Alice anafuatilia jibu lake kwa Chongameno na pindi tu anapopewa jibu ambalo siyo la kuridhisha kwake anaamua kuchoma moto msitu wa Suwerwa (uk. 29). Hatima ya kutofanikiwa kwa msako wake ni kuamua kujiua (uk. 72). Katika fasihi ya watoto hukusudiwa kuwapo na msako ambao mwisho huwa ni kufanikiwa kwa mhusika katika jambo analolifanyia msako. Hatima ya Alice Kesho katika msako wake hakufanikiwa katika kile alichokuwa anakisaka.

Kutokana na maelezo hayo na ushahidi huo, tunaweza kuhitimisha pia kuwa sifa hii nayo inakosekana katika kitabu hiki, maana hata malengo ya msako tunayoambiwa hutarajiwa kuwa na mwisho mwema au mafanikio. Kwa bahati mbaya sana mwisho wa msako huu ni kutofanikiwa; ni majonzi tu.

Hitimisho

Kwa hakika, kutokana na uchambuzi huo uliofanyika, hapana mashaka yoyote kwamba kazi hii ya *Mgomba Changaraweni* haistahili kuingizwa katika kundi la fasihi ya watoto hususan kwa kuzingatia vigezo/sifa/nduni mbalimbali vilivyobainishwa na wataalam mbalimbali kama mwega wa fasihi ya watoto. Kazi hii inapaswa kuingizwa katika fasihi ya watu wazima. Sababu za kutokubaliana kazi hii kuingizwa katika kundi la vitabu vya fasihi ya watoto linatokana na sifa bainishwa kutojitokeza katika kitabu hiki kama tulivyoonyesha katika kurasa zilizotangulia licha ya kutambuliwa na wataalam wengi kuwa ni fasihi ya watoto. Katika mawasiliano kwa njia ya *Whatsaap* (mtandao sogozi) na mwandishi wa kitabu hiki ambaye kwa sasa ni marehemu (Ken Walibora, 2019) alikiri kuwa kitabu cha *Mgomba Changaraweni* na kile cha *Ahsante ya Punda* ni miongoni mwa vitabu vyake vya fasihi ya watoto. Vilevile, hata Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ya Jamhuri ya Kenya (2015:151) imekiorodhesha kitabu hiki kuwa miongoni mwa vitabu vinavyopaswa kusomwa katika shule za awali na Vyuo vya Mafunzo ya Walimu kwa darasa la 7 na 8. Wambua (2007) naye katika tasnifu yake ya kutosheleza baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Ergeton, miongoni mwa vitabu vitatu alivyovitumia katika

utafiti wake kama sehemu ya fasihi ya watoto ni pamoja na kitabu hiki cha *Mgomba Changaraweni*. Vitabu vingine alivyovitumia kama fasihi ya watoto mbali na *Mgomba Changaraweni* ni *Mtu wa Mvua na Ndoto ya Amerika* vyote vikiwa vimeandikwa na Ken Walibora.

Kwa hivyo basi, tunaonelea ipo haja kwa wataalam, waandishi wa kazi za fasihi ya watoto, wizara na taasisi zinazohusika na uainishaji wa vitabu, kuchunguza kwa makini vitabu husika kabla ya kuviteua kutumika na kundi fulani la wahusika. Kulichunguza suala hili kwa umakini na kulifanyia kazi kutasaidia kuhakikisha kazi husika zinawekwa katika kundi lake husika kama inavyostahili.

Marejeleo

Bakize, Leonard H. 2014. *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Bakize, Leonard H. 2015. Gender Balance Struggles in Tanzanian Swahili Children's Literature. *Kiswahili*, Juz. 78, Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Kur. 59-66.

Introduction to the World of Children's Literature (n.d.) retrieved from https://www.pearsonhighered.com

Kahigi, Kulikoyela K. 1995. Lugha katika Vitabu vya Watoto. *Kioo cha Lugha*, Juz. 10. Dar es Salaam: Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Kur. 122-134.

Kenya's Ministry of Education, Science and Technology. 2015. Approved List of School Textbooks and other Instructional Materials for ECDE, Primary Schools and Teacher Training Colleges; revised 14th Edition, Volume one.

Lyimo, Edith B. 2014. Nduni za Fasihi ya Watoto: Mifano Kutoka katika Vitabu vya Kiswahili vya Fasihi ya Watoto nchini Tanzania. *Mulika*, Na. 33, Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Kur. 33-43.

Lynch-Brown, Carol, Carl M. Tomlinson, and Kathy G. Short. 2014. *Essentials of Children's Literature*, 7th Edition. Edinburgh: Pearson Education Limited.

Matundura, Enock, John M. Kobia, Mwenda Mukuthuria. 2013. Taswira Dumifu za Uana katika Fasihi ya Kiswahili ya Watoto. *Mulika*, Na. 32, Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Kur. 28-46.

Medical Aid Foundation. 1995. *Kilio Chetu.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mulokozi, Mugyabuso M. 2017. *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Ngugi, Pamela Muhadia Yalwala. 2011. Ufundishaji wa Fasihi ya Watoto katika Shule za Msingi Nchini Kenya. *Kioo cha Lugha*, Juz. 9. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kur. 84-94.

Ngugi, Pamela Muhadia Yalwala. 2012. Tafsiri katika Fasihi ya Watoto: Mbinu na Mikakati. *Mulika*, Na. 31. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kur. 13-24.

Schneider, Jenifer Jasisnski. 2016. *The inside, outside, and upside downs of children's literature: From poets and pop-ups to princesses and porridge*. Digital Commons@ University of South Florida.

Senkoro, Fikeni. E. M. K. 2006. Fasihi ya Kiswahili ya Majaribio: Makutano ya Fasihi Simulizi na Andishi. *Kioo cha Lugha*, Juzuu 4. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kur. 22-38.

Stakić, Mirjana. 2014. The Specifics of Children's Literature in the Context of Genre Classification. *Mediterranean Journal of Sciences*, Vol. 5 No. 19, Rome: MCSER Publishing. pp. 243-251.

Wambua, Kyeu David. 2007. *Umwafaka wa Fasihi ya Watoto kwa Misingi ya Mwitikio wa Mtoto Msomaji: Mfano wa Vitabu Vitatu Vilivyoandikwa na Ken Walibora*. (Haijachapishwa) Tasnifu kwa ajili ya Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Egerton.

Wamitila, Kyallo Wadi. 2010. *Kanzi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Vide~Muwa Publisher Limited.